

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO**

Simu: +25526-230081
Nukushi: +25526-2321170
Barua pepe: km@habari.go.tz
Tovuti: www.habari.go.tz



Mji wa Serikali Mtumba,
Mtaa wa Habari,
P.O. Box 25,
40481 DODOMA.

TAARIFA KWA UMMA

UTARATIBU WA UENDESHAJI LIGI ZA SOKA NA MICHEZO MINGINE HAPA NCHINI

Dar es Salaam, Mei 31, 2020:

Kufuatia maelekezo ya Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuruhusu michezo mbalimbali nchini kuendelea kuanzia kesho Juni Mosi, 2020 baada ya kusimamishwa kutokana na kuenea kwa Virusi vya Corona, Serikali imekuwa ikipokea maoni mbalimbali kutoka kwa wadau hususani namna ya kurejesha ligi kuu za soka nchini.

Awali wadau wa soka walikuwa na maoni kwamba ligi za soka zirejee kwa timu kukaa katika kituo kimoja na mashabiki wasiwepo. Wadau wa michezo mingine pia wamekuwa wakiomba utaratibu wa kufuatwa kwa kuzingatia kanuni za afya na umahususi wa michezo husika.

Kutokana na maoni mbalimbali mapya ya wadau wa michezo, wataalamu wa afya na kwa kuzingatia ukweli kwamba maambukizi na wagonjwa wa Homa Kali ya Mapafu (Covid-19) yameendelea kupungua nchini, Serikali inatoa maelekezo yafuatayo:

- 1. Kuzingatia Mwongozo wa Afya Michezoni:** Serikali kupitia Wizara zenye dhamana na Afya na Michezo ilishatoa mwongozo wa Mei 28, 2020 unaoelekeza hatua za kuchukuliwa katika kila hatua za kuendesha michezo nchini. Mwongozo huu umeshasambazwa na uzingatiwe kikamilifu na kila mdau aliyetajwa;
- 2. Kuhusu Mtindo wa Uendeshaji wa Ligi za Soka:** Serikali inaruhusu ligi za soka ambazo kikanuni timu zinatakiwa kucheza nyumbani na ugenini utaratibu huo wa nyumbani na ugenini, badala ya kituo kimoja, uendeleo kutumika. Mwongozo wa Afya uzingatiwe ikiwemo namna ya timu kusafiri, kuweka kambi na kufanya mazoezi zikiwa maeneo mbalimbali nchini;
- 3. Kuhusu mashabiki:** Serikali imeridhia ligi zote za soka na michezo mingine iliyoruhusiwa kurejea, mashabiki watakaotaka kuhudhuria viwanjani waruhusiwe kwa taratibu za kawaida isipokuwa tu kwa michezo

itakazotathminiwa huenda ikajaza viwanja ambapo kanuni ya kuruhusiwa mashabiki wasiozidi nusu ya uwezo wa uwanja itumike na isimamiwe ipasavyo.

Fauka ya hayo, mashabiki wenyewe, viongozi wa vilabu, vyama husika, watendaji wa Serikali katika maeneo husika watalazimika kuhakikisha maelekezo yote ya Mwongozo wa Afya Michezoni yanatekelezwa na kusimamiwa kikamilifu ikiwemo: kuhakikisha hakuna misongamano yoyote wakati wa mashabiki kuingia na kutoka viwanjani; viwanjani watu wakae na kushangilia kwa kuachiana nafasi mita moja; kuvaa barakoa; kunawa kwa sababu na maji tiririka au vipukusi (sanitizer) kabla ya kuingia viwanjani. Hatua kali zichukuliwe kwa watakaokaidi taratibu hizi;

4. **Maelekezo ya Jumla:** Baraza la Michezo la Taifa (BMT), kwa kuzingatia Mwongozo wa Afya Michezoni, liendeleo kuratibu utekelezaji wa maelekezo haya ikiwemo kufanya tathmini na kutoa maelekezo mahsusi juu ya namna ya urejeshaji wa michezo mbalimbali kadiri inavyozidi kurejea hapa nchini kwa kuzingatia aina ya michezo hiyo na masuala ya kiafya ya kuzingatiwa; na
5. **Tahadhari Kuhusu Covid-19:** Serikali inasisitiza kuwa pamoja na maambukizi na wagonjwa kupungua sana nchini, jambo ambalo tunaendelea kumshukuru Mwenyezi Mungu, viongozi wakuu wa nchi kwa miongozo yao, wataalamu wa afya kwa kusimamia kitaalamu na wananchi mbalimbali kwa kutikia na kuchukua hatua, bado ugonjwa wa Covid-19 haujakwisha kabisa hapa nchini na duniani kote, hivyo kila mwanamichezo mmoja mmoja na kila kiongozi wa michezo nchini atapaswa kujilinda na kuwalinda wengine kwa kutekeleza ipasavyo miongozo ya afya na kuwasikiliza wataalamu husika.

Tanbihi: kwa maelekezo haya, Serikali inawatakia wanamichezo wote nchini msimu mwingine adhimu wenye msisimko, burudani na mafanikio mema katika mashindano mbalimbali. Mwongozo kuhusu taratibu za afya michezoni unapatikana kwenye tovuti; www.habari.go.tz.

Imetolewa na:



Dkt. Hassan Abbasi

KATIBU MKUU NA MSEMAJI MKUU WA SERIKALI